


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Simu Na: +255 (026) 2963630
Nukushi: +255 (026) 2963629
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz

Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>



Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Utumishi,
S.L.P 670,
DODOMA.

Mtumba, DODOMA
23 Agosti, 2023

TAARIFA KWA UMMA

UPOTOSHAJI KUHUSU KURUDISHWA KAZINI KWA WATUMISHI
WALIOSIMAMISHWA/KUFUKUZWA KAZI SERIKALINI

Kumekuwa na mfululizo wa uandaaji na usambazaji wa taarifa za upotoshaji kwenye mitandao ya kijamii kuhusu urejeshwaji wa watumishi walioondolewa kwenye utumishi wa umma kwa kosa la kughushi vyeti na waliosimamishwa kazi kwa kutokuwa na cheti cha kidato cha nne mwaka 2017-2019.

Wapotoshaji hao wanawataka watumishi waliosimamishwa/kufukuzwa kazi Serikalini kuwasilisha nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na *nakala ya barua ya kushinda rufaa, kitambulisho cha NIDA, barua ya kuthibitishwa kazini, salary slip na barua ya kusimamishwa/kufukuzwa kazi na wanaombwa kutoa kiwango fulani cha fedha kadri ya makubalinano ili warudishwe kazini.*

Aidha, matapeli hao wamekuwa wakibadili tarehe ya taarifa yao kwa umma na kuacha maudhui yakiwa ya aina moja na kuwataka Watumishi husika kuwasiliana nao kwa namba za simu ya mkononi +255627416394, +255621886163 au +255735051419 kwa lengo la kujipatia kipato kwa njia ya udanganyifu.

Hivyo, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inawasisitiza Watumishi wa Umma na wananchi kwa jumla kuwa makini na taarifa hizo kwa kuwa Serikali ina njia na utaratibu rasmi wa kutoa taarifa kwa wadau wake na sio utaratibu unaotumiwa na wapotoshaji hao.

Aidha, Serikali inatoa onyo kwa wapotoshaji hao kuacha tabia hiyo kwani kupitia vyombo yake vya dola inaendelea kufuatilia ili kuwabaini na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa Sheria.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Mary L. Mwakapenda'.

Mary L. Mwakapenda

MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI (UTUMISHI)